MEI 2018

# Uhifadhi wa Misitu Katika Milima ya Tao la Mashariki kwa ajili ya Uhai wa Ukanda wa Kilimo wa SAGCOT

EASTERN ARC MOUNTAINS CONSERVATION ENDOWMENT FUND
EAMCEF
MFUKO WA HIFADHI YA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI

**UJUMBE MUHIMU**

- Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki huleta uhakika wa upatikananji wa huduma ya maji kwa watumiaji walioko nyanda za chini katika ukanda wa kilimo wa SAGCOT. Eneo la Ukanda wa Kilimo wa SAGCOT limeingia ndani ya eneo la milima minane kati ya ile inayounda Milima ya Tao la Mashariki – Nguu, Nguru, Uluguru, Ukaguru, Rebeho, Malundwe, Udzungwa na Mahenge.
- Unahitajika ubia wa kimkakati kati ya mamlaka za umma na zile binafsi ili kuwezesha uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki.
- Ubia wa kimkakati unaojumuisha Taasisi ya EAMCEF na wawekezaji wa ukanda wa SAGCOT unaweza kusaidia katika jitihada za kutafuta ufadhili kwa pamoja, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mpango wa kulipia huduma zitokanazo na mazingira 'Payment for Ecosystem Services (PES)'

## Utangulizi na maelezo kwa ufupi

Kumekuwa na jitihada mbalimbali za kubadili sekta ya kilimo nchini Tanzania – Kauli mbiu ya 'Kilimo Kwanza' ikiwa ni mojawapo ya jitihada za hivi karibuni zilizorasimishwa mwaka 2009. Kilimo Kwanza kama kauli mbiu ya taifa ya kuchochea mabadiliko ya kilimo nchini ilizinduliwa kama mkusanyiko wa sera na shughuli za kimkakati zitakazosaidia kutatua changamoto mbalimbali katika sekta ya kilimo, na wakati huo huo ikichukuliwa kuwa ni nguzo muhimu katika kufikia Dira ya Taifa ya 2025. Mwaka mmoja baadae, Mei 2010, wakati wa Kongamano la Kidunia la Uchumi katika Africa, ulizinduliwa ubia wa kimataifa wa sekta binafsi ulioitwa 'Kilimo Kwanza Growth Corridors' ili kuvuta ubia na uwekezaji binafsi utakaosaidia kwa haraka kufikia malengo ya Kilimo Kwanza na pia kuleta manufaa ya ziada – kama vile, usalama wa chakula, kupunguza umasikini na kupunguza hatari za kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Ili kuanzisha ubia na uwekezaji binafsi, eneo lenye ukubwa sawa na theluthi moja ya eneo lote la Tanzania Bara (sawa na kilomita za mraba 287,000) lilionekana kufaa kwa ajili ya shoroba (corridor) ya kuendeleza Kilimo Kwanza iliyoitwa "Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)" yaani ukanda wa kukuza kilimo Kusini mwa Tanzania. Dira ya uwekezaji (investment Blue Print) kwa ajili ya uendelezaji wa SAGCOT iliandaliwa mwaka 2011 kama mwongozo unaoonyesha mahitaji muhimu yatakayowezesha kufungua fursa za kilimo zilizoko katika ukanda wa Kusini, pamoja na kuonyesha fursa za uwekezaji zilizoko katika kanda hii. Dira ya uwekezaji huu ni kuingiza hekari 350,000 za ardhi katika uzalishaji wa kilimo chenye faida kupitia umwagiliaji mkubwa katika kipindi cha miaka 20. Ili kutimiza shughuli hii, mpangilio wa kugawa maeneo katika kongani (clusters) ulikubalika, jumla ya kongani sita zilitambuliwa - Kilombero, Mbarali, Ihemi, Ludewa, Sumbawanga na Rufiji. Andiko la dira ya SAGCOT - yaani SAGCOT Blue Print linatambua kwamba "manufaa ya muda mrefu katika kuendeleza kilimo yatadhoofishwa ikiwa mfumo wa ikolojia na maliasili hazitosimamiwa vizuri". Ijapokuwa utekelezaji wa SAGCOT unatarajiwa kuboresha matumizi ya ardhi, usimamizi wa udongo na maji katika kila kongani, kwa mfano kwa kulima kilimo mseto cha miti na mazao, usimamizi wa rutuba ya udongo, uvunaji wa maji, uhifadhi wa unyevu ardhini na ulimaji usioharibu udongo – andiko la Blue Print halikutoa mpango wa kina kuhusu utekelezaji wa masuala hayo.

Ili kuboresha andiko la SAGCOT na kuhakikisha kuwa maendeleo tarajiwa katika shoroba hii ni rafiki kwa mazingira, yanayozingatia jamii na yenye faida kiuchumi, andiko la Blue Print liliongezewa nguvu na andiko lingine la kimkakati linalojulikana kama "The Green Print" la mwaka 2012. Andiko la The Green Print linabainisha mikakati ya kutekeleza Ukuaji wa Kilimo cha Kijani "Agriculture Green Growth (AGG)"– kwa kuongeza uzalishaji lakini wakati huo huo kuhakikisha uhifadhi wa maliasili, kupunguza uharibifu wa misitu, rasilimali za maji na bioanuwai. Katika Sura ya nne ya andiko la Green Print, shughuli maalumu zimeainishwa, ambazo ni za uwekezaji na miradi zinazopaswa kutekelezwa na kuhamasishwa ili kutekeleza dhana ya AGG katika shughuli za SAGCOT.

## Kuna uhusiano gani kati ya Milima ya Tao la Mashariki na Programu ya SAGCOT?

Milima ya Tao la Mashariki imesambaa kuanzia Kusini mwa Tanzania mpaka Kusini-Mashariki mwa Kenya, ikiwa na eneo la kilomita za mraba 23,000 – zikiundwa na milima ya Upare (Kaskazini na Kusini), Usambara (Magharibi na Mashariki), Nguu, Nguru, Ukaguru, Uluguru, Malundwe, Rubeho, Udzungwa na Mahenge kwa upande wa Tanzania pamoja na Vilima vya Taita kwa upande wa Kenya. Eneo la SAGCOT linaingiliana katika milima minane kati ya ile inayounda Milima ya Tao la Mashariki – Nguu, Nguru, Uluguru, Ukaguru, Rebeho, Malundwe, Udzungwa na Mahenge (angalia kielelezo katika ramani namba 1). Miongoni mwa huduma mbalimbali, Milima hii ni Malindi-maji (watershed) yanayotiririsha maji kuelekea kwenye mabonde ya mito na maeneo oevu katika eneo kubwa la SAGCOT – kwa mfano bonde la mto Ruaha/Rufiji lenye mapokeleo makuu ya maji matatu ya Ruaha Mkuu, Kilombero na eneo oevu la Luwego lililoko katika bonde la Kilombero, bonde la Usangu na Delta ya

Rufiji yote imesambaa katika eneo la SAGCOT, ikitoa huduma kwa eneo kubwa. Baadhi ya mito mingine muhimu katika eneo la SAGCOT ni Wami/Bonde la Ruvu, Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa.

Milima ya Tao la Mashariki ni chanzo cha maji nchini, ikiwamo eneo la SAGCOT – zaidi ya asilimia 90 ya umeme wa maji unaozalishwa katika vituo vikubwa – kwa mfano, mito inayotoka katika Milima ya Udzungwa hupeleka maji yake katika vituo vya uzalishaji umeme vya Kidatu na Mtera (vyote vikiwa ndani ya Mto Ruaha Mkuu), na kituo cha Kihansi (kilichopo katika mto Kihansi). Milima ya Pare kaskazini, Kusini na Usambara Magharibi hupeleka maji kwenye maporomoko ya Pangani na kituo cha uzalishaji umeme cha Hale na Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Ukiachilia mbali vituo hivyo vya kuzalisha umeme, mpango mkakati wa nishati wa serikali wa mwaka 2016 umeorodhesha ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme katika bonde la Stiegler (Stiegler's Gorge) ifikapo 2035. Bonde hili hupokea maji kutoka katika Mto Ruaha Mkuu, na bwawa litakalojengwa linategemewa kuendesha mitambo ya kufua umeme yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 2100 za umeme.


## Maeneo Muhimu ya Mashirikiano kati ya EAMCEF na SAGCOT

Andiko la SAGCOT la Green Print linaainisha uwekezaji katika misitu, maji na nishati-hai (bioenergy) na kama mojawapo ya mikakati ya kufikia lengo la Kilimo cha Kijani (AGG) kwa kuwa rasilimali hizo ndizo tegemeo kwa uhai wa SAGCOT. Mikakati iliyopendekezwa ni pamoja na; uhifadhi wa kibiashara wa misitu ya jamii, ulipiaji wa huduma za mfumo wa kiikolojia, nishati-hai, na usimamizi bora wa maji ili kuhakikisha ufanisi katika matumizi na ugawanaji wa maji miongoni mwa wadau mbalimbali, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa maji kwa usimamizi madhubuti wa malindi-maji/vyanzo vya maji.

Katika uwanda huu ambapo eneo la SAGCOT limeainishwa, serikali ilishaanzisha Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki – yaani Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund (EAMCEF) tangu mwaka 2001. Mfuko huu ulianzishwa na serikali kama mfuko ambao utatumika kupitisha fedha kwa ajili ya kuhakikisha uhifadhi wa muda mrefu wa mfumo wa ikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki. EAMCEF inahifadhi milima hii kwa ajili ya vyanzo vya maji, bioanuwai na uhifadhi wa ardhi/udongo. Hivi karibuni katika mwaka 2016, taasisi ya EAMCEF ilikamilisha utekelezaji wa mradi wa uhifadhi wa miaka mitano (2011-2016) uliofadhiliwa na Serikali ya Norway iliyotoa ruzuku takribani Dola za Kimarekani Milioni 5.95 ili kuboresha uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki, ikilenga maeneo tisa ya Hifadhi yaliyopewa kipaumbele - maeneo manane yakiwa ni Misitu ya Hifadhi za Asili za Amani, Nilo, Magamba, Chome, Uluguru, Mkingu, Kilombero na Uzungwa Scarp na eneo moja lilikuwa katika Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa.

Mradi huu wa miaka mitano uliotekelezwa na EAMCEF ulipata matokeo makubwa yaliyoshawishi ufadhili wa awamu ya pili ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2016-2019 kwa bajeti ya Dola za Kimarekani Milioni 3.125. Shughuli za EAMCEF za uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki ni jitihada muhimu zinazohakikisha uendelevu wa muda mrefu (au uhai) wa ukanda huu wa kilimo wa SAGCOT na hivyo kuchangia katika kufikia adhma ya andiko la Green Print. Kwa kuwa EAMCEF imeshaanzishwa na imeshadhihirisha uwezo mkubwa wa kuongoza utekelezaji wa mradi mkubwa wa uhifadhi kupitia ushirikishwaji wa wanajamii, ubia wa kimkakati na SAGCOT unahitajika ili kufikia malengo ya andiko la Green Print.

Kutokana na aina ya ubia utakaojengwa, taasisi ya EAMCEF na sekta binafsi zinaweza kushirikiana kwa pamoja katika kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi itakayowezesha usimamizi endelevu wa ikolojia – fedha hizo zinaweza kupitishiwa katika Mfuko huu wa EAMCEF. Vile vile, unaweza kuandaliwa mfumo madhubuti wa ulipiaji wa huduma zitolewazo na mazingira 'Payment for Ecosystem Services' unaoshirikisha taasisi binafsi na wadau wengine wa eneo la SAGCOT ili kufidia jamii zilizoko katika maeneo ya hifadhi na zinazojihusisha katika kutunza maeneo hayo, pamoja na taasisi zinazosimamia Maeneo ya Hifadhi husika.








### Kuhusu EAMCEF

Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki, yaani Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund (EAMCEF) ni mfuko wa udhamini ulioanzishwa na unaofanya kazi kama mfumo wa muda mrefu na wa uhakika wa ufadhili wa maendeleo ya jamii, tafiti za uhifadhi na kuendeleza bioanuwai, huduma za kiikolojia na matumizi endelevu ya maliasili katika Milima ya Tao la Mashariki iliyoko upande wa Tanzania. Tasisi ya EAMCEF ilisajiliwa rasmi nchini Tanzania mnamo tarehe 6 Juni 2001 na inaendeshwa kama asasi inayojitegemea na isiyolenga katika kujizalishia faida.

### Dira

Dira yetu ni kuona kuwa Milima ya Tao la Mashariki na watu wanaotegemea milima hiyo vinaishi katika hali ya amani kama mfumo mmoja wa kiikolojia ulio endelevu. Misitu na milima itatoa mazao yake na huduma mbalimbali – kutoka maji mpaka umeme, kutoka chakula na mazao ya biashara mpaka madawa – kwa ajili ya watu wa Tanzania. Na jamii ya ulimwengu inanufaika kwa uwepo wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya bioanuwai na hifadhi kubwa ya kaboni inayopunguza ongezeko la joto la dunia.

### Dhima

Dhima yetu ni kuwezesha upatikanaji wa rasilimali ili kusaidia uhifadhi wa bioanuwai za misitu katika Milima ya Tao la Mashariki iliyopo upande wa Tanzania kupitia uwekezaji katika maendeleo ya jamii na uboreshaji wa hali za maisha, ufadhili wa kudumu kwa ajili ya usimamizi wa maeneo ya hifadhi na msaada wa kifedha kwa ajili ya tafiti za bionuwai na mabadiliko ya tabianchi.

### Milima ya Tao la Mashariki iliyopo Tanzania

Milima ya Tao la Mashariki iliyopo Tanzania imesambaa katika eneo la Kilomita za mraba takribani 5,350. Milima mikuu ya Tao la Mashariki imesambaa katika zaidi ya Wilaya kumi na tano za mikoa mitano ya Tanzania, ambayo ni; Tanga (Milima ya Usambara Mashariki na Magharibi, na Milima ya Nguu), Kilimanjaro (Milima ya Upare Kaskazini na Kusini), Morogoro (Milima ya Nguru, Uluguru, Ukaguru, Udzungwa, malundwe, Mahenge na Rubeho), Dodoma (Milima ya Rubeho) na Iringa (Milima ya Udzungwa).

### Maeneo Makuu ya kazi

1. Uhifadhi shirikishi wa jamii na shughuli za maendeleo kwa ajili ya kuboresha maisha ya jamii za vijijini zinazoishi pembezoni mwa maeneo ya misitu lengwa.
2. Tafiti za bioanuwai zinazofaa kwa ajili ya uhifadhi wa bioanuwai katika baadhi ya Milima ya Tao la Mashariki
3. Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi na Mabadiliko ya Tabianchi ili kuboresha shughuli za kiikolojia na kuimarisha uwezo wa taasis husika katika usimamizi.

Andiko hili limeandaliwa kutoka kwenye Ripoti ya Matokeo ya Mradi wa Kuboresha Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki iliyoko upande wa Tanzania 'Improving Conservation of the Eastern Arc Mountains of Tanzania' (2011-2016

Kwa taarifa zaidi, wasiliana na:

Sekretarieti ya Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki
Kitalu Na.348, Eneo la Forest Hill, Barabara ya Kingalu,
S.L.P 6053,
Morogoro, TANZANIA.

+255 23 293 4274 | +255 755 330 558 | +255 23 293 4273

eamcef@easternarc.or.tz | www.easternarc.or.tz